



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS



TAWALA LA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKO NA KILIMANJARO

Simu : 27- 29 74369
Fax : 27- 29 74368
Email: ded@haidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
S.L.P. 27,

HAI.
Tarehe: 29/03/2022.

TANGAZO - LINARUDIWA

TANGAZO LA KUTAFUTA FUNDI (Local Fundi) KWA AJILI YA KAZI YA UJENZI WA JENGU LA KUIFADHIA MAITI (MORTUARY), SHIMO LA KUHIFADHIA KONDO LA NYUMA (PLACENTA PIT), SEPTIC TANK NA SOAKWAY PIT KATIKA KITUO CHA AFYA LONGOI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai amepata fedha toka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuifadhia maiti (Mortuary), na shimo la kuhifadhia kondo la nyuma (Placenta pit).septic tank, soakway pit Napenda kuwatangazia mafundi wote (Local fundi) wenye uwezo wa kujenga majengo ya serikali wajitokeze na kuomba kazi hii.

Mafundi wenye sifa na uzoefu wanatakiwa kuja kuchukua fomu maalumu(schedule of labour) katika ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kwa ajili ya kujaza bei za ujenzi huo.

Sifa za Mwombaji.

1. Awe ni raia wa Tanzania mwenye uelewa mzuri wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza
2. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.
3. Awe na uelewa mzuri wa usalama na Afya awapo eneo la kazi.
4. Awe na timu ya kutosha ya mafundi mbalimbali kwa muda wote wa kazi mfano fundi mwashi,fundi bomba ,fundi umeme,fundi carpenta nk.
5. Awe na uwezo wa kuandaa na kutekeleza mpango kazi wa mradi /miradi na kumaliza kwa wakati.
6. Awe mwadilifu na mwaminifu.
7. Uwezo wa kusimamia mafundi wenzake na vibarua.
8. Mwenye zana zote muhimu za kazi (tools).
9. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri mchoro/michoro ya majengo kwa lugha ya kiufundi.

10. Ada ya maombi ya kazi ya ufundi ni shilingi elfu ishirini (20,000/=) kwa kila kazi, fedha hii haitarudishwa (non-refundable fee of application).

Uzoefu.

1. Uzoefu wa kuanzia walau miaka miwili na kuendelea katika kazi ya ujenzi.
2. Awe amefanya kazi yoyote ya ujenzi /ukarabati wa majengo ya serikali walau miradi miwili na hati ya huduma (**certificate of service**) au mikataba ya miradi iliyoteklezwa ambayo inafikika kwa uthibitisho (ambatanisha uthibitisho).
3. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri mchoro/michoro ya majengo kwa lugha ya kiufundi.

AMBATANISHA VITU VIFUATAVYO:

1. Kitambulisho cha Taifa, kadi ya mpiga kura au leseni ya udereva au kitambulisho chochote kinacho julikana kiserikali
2. Mikataba na “certificate” za kazi za serikali ambazo umeshazifanya.
3. “Bank Statement” (Taarifa za bank).
4. Orodha ya mafundi ulionao katika kila fani ya Ujenzi,

Maombi yote yawekwe katika bahasha iliyofungwa vizuri na kuandikwa anuani ifuatayo, Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri (W) Hai.S.L.P 27 Hai.

Mwisho wa kupokea maombi haya ni saa nne kamili (04:00) Asubuhi siku ya jumatatu ya tarehe **05/04/2022** sehemu ya kuwasilisha maombi hayo ni ofisi za Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Hai (Kitengo cha Manunuzi na Ugavi) S.L.P 27 HAI. Ufunguzi wa maombi hayo utafanyika tarehe **05/04/2022**/ mara baada ya kufunga zoezi la kupokea zabuni hizo katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya mbele ya waombaji/ waakilishi watakaopenda kuhudhuria ufunguzi huo.

Tangazo limetolewa na



Rajabu Yateri.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)
HALMASHAURI YA WILAYA-HAI.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HAI